# BODI YA KOROSHO TANZANIA

## TANGAZO LA MKUTANO MKUU WA WADAU WA TASNIA YA KOROSHO MWAKA 2025

Bodi ya Korosho Tanzania inapenda kuwaarifu Wadau wote wa Tasnia ya korosho nchini kuwa mkutano mkuu wa Wadau wa Tasnia ya korosho utafanyika tarehe 21 na 22 Agosti mwaka 2025 kuanzia saa 2 kamili asubuhi katika ukumbi wa Morena Hotel Manispaa ya Morogoro.

Mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hussein M. Bashe (MB). Mada mbalimbali zinazohusu maendeleo ya Tasnia ya Korosho nchini zitawasilishwa na kujadiliwa.

Barua za mwaliko zimetumwa kwa waalikwa wote. Waalikwa wanaombwa kujigharamia usafiri, malazi na gharama zingine. Bodi ya korosho itagharamia chakula na viburudisho wakati wa Mkutano.

Aidha, mkutano huu ni kwa wadau waliopata barua za mwaliko pekee. Kila mshiriki afike na barua yake ya mwaliko. Asiye na barua ya mwaliko hataruhusiwa kushiriki mkutano huo.

Imetolewa na:

**MKURUGENZI MKUU**

**BODI YA KOROSHO TANZANIA**

**S. L. P. BOX 533**

**MTWARA**